BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** sifa zote njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa Rehma, kwa kutujaalia uzima na afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena siku ya leo kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Vile vile, nachukuwa fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi wake ambayo imetuthibitishia kuwa yeye ni kiongozi bora, mchapa kazi na asieyumbishwa na yeyote katika hatua za kupigania haki za wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,** Shukurani za kipekee ziende kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Mheshimiwa Jamal Kassim Ali kwa umahiri wake unaomfanya kuongoza vyema Ofisi hii pamoja na kuwapongeza watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Saleh Juma Mussa pamoja na Afisa Mdhamin Pemba

Ndugu Shuwekha Abdallah Omar kwa kuwa na mashirikiano makubwa na Kamati wakati wote wa ufuatiliaji wa shughuli za Bajeti ya taasisi zilizochini ya Ofisi hii, Aidha, nitakuwa mkosefu wa fadhila iwapo nitawasahau watendaji wa Ofisi ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupata wakati wa kupitia Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Mtumizi ya Fedha ya Mwaka 2023/2024 kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais Ikulu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upekee nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni Wajumbe mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinishwa kwa Ofisi hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya hali ya juu kabisa napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *8.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo kwa ruhusa yako na kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) na 107(3) katika Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya

Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa  ya Baraza la Wawakilishi kuhusu bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Ikulu kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais Ikulu, katika kusimamia na kutekeleza Bajeti yake ina jumla ya Mafungu manne *(4)* ambayo ni Fungu *A 01* – Ofisi ya Rais Ikulu, Fungu *A O2* – Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, Fungu A 09 – Taasisi ya Rais ya usimamizi na Ufuatiliaji wa Utekelezaji Serikalini na Fungu *A 10* – Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imepitia Fungu baada ya Fungu kwa ajili ya kupata ufafanuzi na hatimae kuridhia jumla ya fedha zote ambazo zinakusudiwa kutekeleza jumla ya Programu Kuu Nne. Maelezo ya kina ya programu hizo yametolewa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja kitabu cha Bajeti cha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha cha mwaka 2023/2024.

### *FUNGU A 01:* OFISI YA RAIS IKULU

**Mheshimiwa Spika,** katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha *2023/2024,* Kamati yangu inapenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi maalumu kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa moyo wake wa kuwajali wananchi wa Zanzibar kwa kitendo chake cha kuongeza kiwango cha Pencheni kwa wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na pia kuongeza kiwango cha Pencheni jamii kutoka Tsh. 20,000/= hadi Tsh 50,000/= ni cha kizalendo na cha kupongezwa sana kwa kuwa hatua hii sasa itakwenda kuwainua wazee wetu kutekeleza mahitaji yao kwa namna bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kamati imeridhika na hali ya utulivu na amani katika nchi yetu, hali ambayo inatoa nafasi kwa wananchi na wawekezaji kufanya shughuli zao bila ya hofu yoyote. Hakika tunamshukuru na tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumuongoza katika kila hatua.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kifungu **PA0103** Programu Kuu **Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu**, Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka Mazingira mazuri ya kuimarisha hali ya ulinzi na usalama kwa kujenga uzio wa ukuta na kuweka kamera maalumu za usalama katika Makaazi ya Mheshimiwa Raisi yaliopo Dodoma kutokana na matengenezo ambayo yanaendelea, kufanya hivyo kutazidisha uhakika wa usalama kwa kipindi chote ambacho Mhe. Rais atakua katika makaazi hayo. Sambamba na hilo, Kamati inashauri kufikiriwa kwa karibu kuwekwa mipango ukarabati mkubwa wa Ikulu ndogo iliyopo Bwefum ili isipoteze haiba yake.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati yangu inampongeza tena Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufanikisha vyema ziara zake za Mikoa na Wilaya zote za Zanzibar kwa madhumuni ya kukagua miradi inayoendelea na pia kusikiliza kero zinazowakabili wananchi wake. Hata hivyo, kupitia fungu dogo la ***SA010103*** la **Usimamizi wa Miradi ya Kimkakati** Kamati tunashauri Serikali kuongeza juhudi na mipango endelevu ya ujenzi wa bandari ya Manga Pwani kwa kuzishirikisha Nchi wahisani au kwa mashirikiano na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwani kutekeleza ujenzi huu ni kuzidi kuifungua Zanzibar kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, utekelezaji wa Programu hii pia, iangazie na barabara ambazo zimeahidiwa kupitia ziara za Mheshimiwa Rais ambapo wananchi walipata fursa ya kutoa maoni yao kupitia kero na changamoto mbali mbali zinazowakabili.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa barabara hizo ni ile ya Birikau Wilaya ya Chake – Chake ambayo ilijengwa na asasi ya kiraia ya Milele Foundation kwa kiwango cha kifusi na kuwekewa lami ya awali na tukumbuke kwamba katika kipindi hiki cha mvua za masika imeshaanza kuharibika kwa kufanya mashimo na kutoka tabaka ya juu yenye lami, hivyo, kupelekea ugumu wa matumizi kwa wananchi wanaotumia barabara hii, lakini pia matengenezo hayo itakuwa ni utekelezaji wa ahadi ya siku nyingi ya Mheshimiwa Raisi kwa wananchi wa maeneo hayo.

***FUNGU A 02:*** **OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaupongeza uongozi wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kupata Ofisi mpya hapo BOSNIA yenye nafasi ya kutosha kwa watendaji wake. Kiujumla Ofisi hii inasimamia Programu Kuu mbili ikiwemo *Usimamizi wa Majukumu ya kikatiba na Kisheria ya BLM* pamoja na programu ya *Utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.* Ni matumaini yetu kuwa kazi zilizopangwa kupitia Programu hizi zitakalimika kwa weledi na malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ukomo mdogo wa fedha za Matumizi Mengineyo ambazo Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imekadiriwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kamati inashauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa wakati ili kuweza kufanikisha shughuli mbali mbali zinazotarajiwa kufanyika kwa wakati unaopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu Kuu ya **Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi** Kamati imeridhika kuona ikitekeleza vyema majukumu yake kwa kusimamia majukumu ya ofisi kama ilivyoainishwa kwa misingi ya Sheria. Kwa kuwa, Program hii imebeba lengo la kuimarisha mazingira bora ya kazi, bidii na kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi na ili kufikia

lengo hili, Kamati yetu inaishauri Serikali kuwaangalia kwa moyo wa huruma watendaji wa ofisi hii kwa kuboresha maslahi yao, sambamba na kuimarishwa kwa mfumo wa mafunzo kutoka ngazi za chini hadi elimu za juu kwa lengo la kuongeza ubora katika utendaji wao.

***FUNGU A 09:* TAASISI YA RAIS YA USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA UTENDAJI SERIKALINI**

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu Kuu ya **Uratibu wa Shughuli na Huduma zinazotolewa Serikalini** yenye malengo ya kuimarisha uratibu na usimamizi kwa uwajibikaji katika utoaji wa huduma bora katika jamii ambapo matarajio yake ni kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya kikanda na kimataifa. Kamati inaipongeza Ofisi hii mpya kwa kuanza vyema kusimamia majukumu yake na kuhakikisha malengo ya ofisi yanafikiwa kama ilivyokusudiwa, ni matarajio yetu kuwa ofisi hii itapatiwa watendaji bora wenye uwezo mkubwa na utaalamu wa fani mbali mbali ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza ahadi yake ya kuleta huduma bora kwa wananchi na vile vile, kumsaidia kuweka miundombinu bora ya maendeleo. Aidha, Kamati inaipongeza ofisi kwa kupata fungu lake la A09 ambalo litaweza kurahisisha utekelezaji wa kazi zake.

***FUNGU A 10:* TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu kwa Bajeti hii ya mwaka 2023/2024 imeweza kuondolewa jukumu la ukusanyaji wa mapato kutokana na ukosefu wa vyanzo vya mapato, ambapo walitakiwa wakusanye kwa kila mwaka hali ambayo ilipelekea kupata uzito kwa utendaji kazi wao. Hata hivyo, Kamati kupitia program ya Uhifadhi na Utunzaji wa Kumbukumbu za Serikali na Umma, tunashauri Taasisi hii kuzidisha kasi ya utendaji kazi

pamoja na kutimiza majukumu yao ambayo yatafanya tuzidi kutambulika kutokana na urithi wa historia ndefu iliyopo Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaipongeza Taasisi hii, kwa kununua nyumba mbili ambazo zipo karibu na Ofisi Kuu ya Kilimani kwa lengo la kutanua eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya ambao utakua ujenzi wa kisasa na wenye kuzingatia wakati tulionao katika sekta ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za Taifa. Sambamba na hayo, Kamati inaliomba Baraza hili tukufu kuidhinisha fedha jumla ya *TSH. Bilioni 3 na Milioni Mia Tano* ambazo zimepangwa kwa ajili ya Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya nyaraka ili zikaweze kutumika kwa wakati na Serikali ihakikishe fedha hizo zimetumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

***HITIMISHO:***

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba yangu, nachukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu. Aidha, Kamati inatoa shukurani zake za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu kwa mashirikiano yake makubwa anayotupatia wakati wote wa ziara za Kamati lakini pia, mashirikiano yake katika kipindi kigumu cha kupitia bajeti ya mafungu ya wizara yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa

ili utekelezaji wa shughuli za kila siku uweze kuendelea na kufikia malengo ya kuleta maendeleo kwa wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie Bajeti hii na hatimae waidhinishe Ofisi ya Rais Ikulu, makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha *2023/2024* kama ulivyo utaratibu wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu

***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

……………………………

(Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu aa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**